FUNZO LA 23

1. Je, aliitwaje mwana ambaye Mungu aliwapa Ibrahamu na Sara?
-Isaka.

2. Je, Ibrahamu alijua kuwa Mungu alipanga kumleta Mwokozi kupitia kizazi cha Isaka?
-Ndiyo.

3. Je, kwanini Mungu alimwamuru Ibrahamu amtoe Isaka sadaka?
-Kwa sababu Mungu alimpa Ibrahamu uhai.
-Kwa sababu Mungu alimpa Isaka uhai.
-Kwa sababu Mungu ni Bwana wa watu wote.

4. Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa Isaka atakuwa baba wa uzao mwingi na kuwa Mwokozi atakuwa mzao wake, je, Mungu alibadilisha mawazo yake?
-La.

5. Je, Ibrahamu aliwaza kuwa Mungu alibadili mawazo yake?
-La.
-Ibrahamu alimwamini Mungu na ahadi zake.

6. Je, Ibrahamu aliamini Mungu angefanya nini kama angemtoa Isaka sadaka?
-Ibrahamu aliamini kuwa kama angemtoa Isaka sadaka, Mungu angemfufua Isaka kutoka kwa wafu.



7. Kwa nini Ibrahamu hangeweza kumuokoa Isaka?
-Kwa sababu Ibrahamu alikuwa tayari amekiinua kisu ili amtoe Isaka sadaka.

8. Kwa nini Isaka hangeweza kujiokoa?
-Kwa sababu Ibrahamu alikuwa ameifunga miguu na mikono ya Isaka.

9. Je, watu wengine wanaweza kutuokoa?
-La.

10. Je, tunaweza kujiokoa?
-La.

11. Je, ni nani pekee anaweza kutuokoa?
-Mungu.

12. Je, ni nani aliyemuongelesha Ibrahamu na kumuokoa Isaka?
-Mungu.

13. Je, ni nani aliyetwaa sadaka ambayo ilichukuwa sehemu ya Isaka?
-Mungu.

14. Je, kwa nini Mungu alimfunga huyo kondoo kwa pembe zake?
-Kwa sababu Mungu angekubali sadaka kamilifu pekee kuchukuwa sehemu ya Isaka.

15. Je, kwa nini Ibrahamu alipaita hapo pahali, “Mungu atatwaa”?
-Ibrahamu aliamini kuwa, kama vile Mungu alivyojitwalia kondoo, hivyo ndivyo atatwaa Mwokozi awaokoe watu.

-Mke wa Ibrahamu Sara akafa, na Isaka akamuomboleza.

-Baada ya mke wa Ibrahamu Sara kufa, Ibrahamu alimfanyia nini Isaka ili kumfariji?

Tusome Mwanzo 24:67 & 25:20

67-Isaka akamwingiza Rebeka katika hema ya mama yake, Sara, akamtwaa Rebeka, akawa mkewe, akampenda; Isaka akafarijika kwa ajili ya kufa kwa mamake.
20-Isaka akawa mwenye miaka arobaini alipomtwaa Rebeka binti Bethueli, Mshami, wa Padan-aramu, ndugu wa Labani, Mshami, kuwa mke wake.

-Ibrahamu alimtafutia mwanawe Isaka mke.

-Je, jina la mke wake Isaka lilikuwa lipi?
-Rebeka.

-Rebeka alizaliwa katika nchi aliyokuwa akiishi Ibrahamu kabla ya Mungu kumuelekeza Kanaani.

-Baada ya muda, pia Ibrahamu alikufa.

-Kwa sababu mke wa Isaka, Rebeka, alikuwa tasa, hangeweza



kupata watoto.

-Lakini Isaka akamwombea, na Mungu akajibu maombi yake.

Tusome Mwanzo 25:21-23

21-Isaka akamwomba Bwana kwa ajili ya mke wake, maana alikuwa tasa. Naye Bwana akamwitikia, na Rebeka mkewe akachukua mimba.
22-Watoto wakashindana tumboni mwake. Naye akasema, Ikiwa ni hivi, kuishi kwanifaa nini? Akaenda kumwuliza Bwana.
23-Bwana akamwambia,Mataifa mawili yamo tumboni mwako,Na kabila mbili za watu watafarakana tangu tumboni mwako.Kabila moja litakuwa hodari kuliko la pili,Na mkubwa atamtumikia mdogo.

-Kabla ya watoto wa Rebeka kuzaliwa, alimuuliza Mungu kuwahusu.
-Mungu alimjibu vipi?

-Mungu alimjibu Rebeka kuwa, atazaa mapacha, na yule mkubwa atamtumikia yule mdogo.

-Kabla ya mapacha wa Rebeka kuzaliwa, Mungu alijua kila kitu kuwahusu.

-Je, Mungu alijuaje kila kitu kuwahusu mapacha wa Rebeka kabla wazaliwe?

-Mungu anajua kila kitu kuhusu watu wote.
-Hakuna kisicho wazi kwa Mungu.

-Kabla tuzaliwe, Mungu anajua kila kitu kutuhusu.

-Mungu anajua yote yaliyotufanyikia awali.
-Mungu anajua kila kitu kinachotufanyikia sasa.
-Mungu anajua kila kitu kitakachotufanyikia usoni.

-Baada ya muda, Rebeka alizaa wana mapacha.

Tusome Mwanzo 25:24-26

24-Siku zake za kuzaa zilipotimia, tazama! Mapacha walikuwamo tumboni mwake.
25-Wa kwanza akatoka, naye alikuwa mwekundu mwili wote kama vazi la nywele. Wakamwita jina lake Esau.
26-Baadaye ndugu yake akatoka, na mkono wake unamshika Esau kisigino. Akaitwa jina lake Yakobo. Isaka alikuwa mwenye miaka sitini mkewe alipowazaa.

-Je, majina ya wavulana mapacha ambao Rebeka alizaa waliitwaje?
-Esau na Yakobo.

-Esau alikuwa wa kwanza.

Tusome Mwanzo 25:27a

27-Watoto wakakua, Esau alikuwa mtu ajuaye kuwinda



wanyama, mtu wa nyikani,

-Esau alikuwa mwindaji hodari, na alitumia muda wake mwingi kuwinda.

-Je, Esau alimwamini Mungu?
-La.

-Yakobo alikuwa mzaliwa wa pili.

Tusome Mwanzo 25:27b

27-Na Yakobo alikuwa mtu mtulivu, mwenye kukaa hemani.

-Yakobo alifuga kondoo na ng'ombe na aliishi kwa utulivu katika hema yake.

-Je, Yakobo alimwamini Mungu?
-Ndiyo.

-Siku moja, jambo fulani lilifanyika kati ya Esau na Yakobo.

Tusome Mwanzo 25:29-34

29-Yakobo akapika chakula cha dengu. Esau akaja kutoka nyikani, naye alikuwa amechoka sana.
30-Esau akamwambia Yakobo, Tafadhali, unipe hicho chakula chekundu nile, kwa sababu ninazimia mimi. Kwa hiyo walimwita jina lake Edomu.

31-Yakobo akamwambia, Kwanza niuzie leo haki yako ya mzaliwa wa kwanza.

32-Esau akasema, Tazama, mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi?

33-Yakobo akamwambia, Uniapie kwanza. Naye akamwapia, akamwuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza.

34-Yakobo akampa Esau mkate na chakula cha dengu, naye akala, akanywa, kisha akaondoka, akaenda zake. Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza.

-Siku moja, Esau alirudi kutoka mawindoni na alikuwa anahisi njaa sana.

-Esau alimwona Yakobo akipika kitoweo cha dengu na akamwambia Yakobo ampe.

-Kwa sababu Esau alikuwa njaa, aliuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza kwa kitoweo cha dengu.

-Je, kwa nini Esau aliuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza?
-Kwa sababu hakuudhamini.

-Je, Esau alidhamini nini?

-Alidhamini tumbo lake tu.
-Esau alidhamini mwili wake tu.

-Je, Esau na Yakobo walikuwa tofauti vipi?



-Esau hakudhani kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Yakobo alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.

-Esau hakudhani kuwa alikuwa mwenye dhambi kwa Mungu.
-Yakobo alijua kuwa alikuwa mwenye dhambi kwa Mungu.

-Esau hakudhani kuwa dhambi huleta kifo cha milele.
-Yakobo alijua kuwa dhambi huleta kifo cha milele.

-Esau hakutaka kumfuata Mungu.
-Yakobo alitaka kumfuata Mungu.

-Esau hakutaka Mungu amtume Mwokozi ili amwokoe.
-Yakobo alitaka Mungu amtume Mwokozi amwokoe.

-Kama mzaliwa wa kwanza, haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa ya Esau.

-Kama mzaliwa wa kwanza, Mungu angemtuma Mwokozi kupitia uzao wa Esau.

-Lakini Esau hakudhamini haki ya uzaliwa wa kwanza.

-Esau hakumtaka Mungu amtume Mwokozi kupitia uzao wake.

-Esau alitaka kitoweo cha dengu tu.
-Esau alitaka kile tumbo lake lilimwambia.

-Je, tunafuata kile matumbo yetu yanatuambia, au tunamfuata Mungu?

-Je, tunafuata kile miili yetu inatuambia, au tunamfuata Mungu?

-Tukifuata tumbo letu, litatuongoza kwa kifo.
-Tukifuata miili yetu, itatuongoza kwa kifo.

-Tukimfuata Mungu, atatuongoza kwa uzima.
-Kwa sababu Esau hakumwamini Mungu, Mungu alimchagua Yakobo.

-Kwa sababu Esau hakumwamini Mungu, Mungu aliamua kumtuma Mwokozi kupitia uzao wa Yakobo.

-Je, kwa nini Mungu aliamua kumtuma mwokozi kupitia uzao wa Yakobo?
-Kwa sababu Esau hakumwamini Mungu.

-Kwa sababu Esau hakumwamini Mungu, Mungu alimpa Yakobo haki ya mzaliwa wa kwanza.

-Mungu alipompa Yakobo haki ya mzaliwa wa kwanza, Esau alikasirika sana.

Tusome Mwanzo 27:41

41-Esau akamchukia Yakobo kwa ajili ya ile baraka babaye aliombarikia. Esau akasema moyoni mwake, Siku za kumlilia baba yangu zinakaribia, ndipo nitakapomuua ndugu yangu Yakobo.

-Esau alimkasirikia Yakobo sana hadi alipanga kumuua.



-Lakini Rebeka mamake Yakobo alisikia kuwa Esau alipanga kumuua Yakobo.

-Kwa hivyo, Rebeka akamuita Yakobo na kumtuma kwenda katika nchi aliyozaliwa.

Tusome Mwanzo 27:42-44

42-Rebeka akaarifiwa maneno ya Esau, mwanawe mkubwa. Akapeleka mtu kumwita Yakobo, mwanawe mdogo, akamwambia, Tazama, katika habari zako Esau, ndugu yako, anajifariji moyo wake, maana anakusudia kukuua.
43-Na sasa, mwanangu, sikia sauti yangu, uondoke, ukimbilie kwa Labani, ndugu yangu huko Harani;
44-ukae kwake siku chache, hata ghadhabu ya ndugu yako igeuke;

-Yakobo akawaacha babake na mamake na kuelekea katika nchi ya Harani.

-Harani ilikuwa nchi ambayo Rebeka, mamake Yakobo alikozaliwa.

-Harani ilikuwa nchi ambayo babu yake Yakobo, Ibrahamu, aliishi kabla ya Mungu kumwelekeza Kanaani.

-Harani ilikuwa mbali sana, Yakobo alisafiri siku nyingi.

-Huo usiku, Yakobo alipolala, Mungu alimpa ndoto.

Tusome Mwanzo 28:10-13a

10-Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani.
11-Akafika mahali fulani akakaa huko usiku kucha,
maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali
pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale
pale.
12-Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamishwa juu
ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika
wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake.
13-Na tazama, Bwana amesimama juu yake.

-Je, Yakobo aliona nini katika ndoto aliyopewa na Mungu?
-Yakobo aliona ngazi.

-Je, sehemu ya chini ya hio ngazi iligusa wapi?
-Sehemu ya chini ya hio ngazi iligusa ardhi.

-Je, sehemu ya juu ya hio ngazi ilielekea wapi?
-Sehemu ya juu ya hio ngazi iligusa mbingu.

-Je, ilimaanisha nini ngazi kugusa ardhi na pia kugusa mbingu?
-Ngazi ilikuwa inaleta mbingu na ardhi pamoja.

-Je, ni nani aliyekuwa juu ya ngazi?
-Mungu.

-Je, ni nani waliokuwa wakipanda na kushuka katika hio ngazi?
-Malaika.



-Je, ilimaanisha nini malaika kupanda na kushuka katika hio ngazi?

-Yakuwa Mungu alitaka kuwa Mungu wa Yakobo.

-Je, kwa nini Mungu alimpa Yakobo hii ndoto?

-Mungu alikuwa akimfundisha Yakobo kuhusu Mwokozi ambaye angekuja.

-Je, Mungu alimfundisha Yakobo nini kuhusu Mwokozi?

-Kama vile ngazi ilivyoleta mbingu na ardhi pamoja, hivyo Mwokozi angewaleta watu wa ardhi pamoja na Mungu wa mbinguni.

-Hapo mwanzo, Mungu alitembea pamoja na Adamu na Hawa.

-Lakini Adamu na Hawa hawakumtii Mungu na wakatenganishwa na Mungu.

-Hakukuwa na njia ya Adamu na Hawa kurejea kwa Mungu.

-Lakini Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi ambaye angewaleta watu wa ardhi pamoja na Mungu wa mbinguni pamoja.

-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu, ili watu na Mungu waweze kutembea na Mungu pamoja.

-Ufuatao ni mfano:

-Patrick na Joseph walikuwa marafiki wa dhati.

-Lakini adui yao aliwachukia wote.
-Huyo adui aliuonea wivu urafiki wao.

-Siku moja, adui akafikiri jinsi ya kuuharibu urafiki wa Patrick na Joseph.

-Adui akamwendea Patrick na kumwambia kuwa Joseph alipanga kumuumiza.

-Patrick akaamini uongo wa adui na wakatengana na rafiki yake Joseph.

-Lakini Joseph alimpenda Patrick na akafikiria jinsi ya kurejesha urafiki wao.

-Patrick akamtuma mwana wake kwa Joseph ili amweleze kuwa ni adui aliyemdanganya.

-Kupitia kwa yule mwana, urafiki wa Patrick na Joseph ulirejea.

-Shetani aliwadanganya Adamu na Hawa, akawatenganisha na Mungu.

-Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi ambaye angewaleta watu na Mungu pamoja.

-Kama vile ngazi ilivyokuwa njia pekee ya kufikia mbingu, hivyo basi Mwokozi ndiyo njia pekee ya kufikia mbingu.



-Katika hio ndoto, Mungu alimwongelesha Yakobo.

Tusome Mwanzo 28:13b-15

13-Akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wa Abrahimu baba yako na Mungu wa Isaka: nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako.

14-Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kaskazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa.

15-Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia.

-Hapo awali, Mungu aliwaongelesha watu kupitia kwa ndoto.

-Siku hizi, Mungu huzungumza na watu wake vipi?

-Siku hizi, mara nyingi Mungu huzungumza na watu wake kupitia kwa Kitabu chake, Biblia.

-Je, kwa nini Mungu alimwongelesha Yakobo?
-Mungu alikuwa akimpa Yakobo ahadi.

-Ahadi aliowapa Abraham na Isaka, pia Mungu alimpa Yakobo.

-Je, Mungu alimuahidi nini Yakobo?

-Mungu aliahidi kuwa Yakobo atakuwa na uzao mwingi.
-Mungu aliahidi kuwa atambariki Yakobo.

-Mungu aliahidi kuwabariki watu wote kwa kumtuma Mwokozi ambaye ni wa uzao wa Yakobo.

-Je, Mungu alisahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi?
-La.
-Mungu hawezi kusahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi.

-Je, kwa nini Mungu hawezi sahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi?

-Kwa sababu Mungu hasahau.
-Kwa sababu Mungu habadiliki.
-Kwa sababu Mungu anatimiza ahadi zake wakati wote.

-Asubuhi iliyofuata, Yakobo aliendelea na safari yake.

Tusome Mwanzo 29:1

1-Kisha Yakobo akashika njia yake, akafika nchi ya wana wa mashariki.

-Yakobo aliendelea na Safari yake, hadi mwishowe akafika Harani.

-Pale Harani, Yakobo aliishi miaka mingi.
-Pale Harani, Yakobo alioa dada wawili na akawa baba wa wana kumi na wawili.

-Baada ya Yakobo kuishi katika nchi ya Harani siku nyingi, Mungu alimwongelesha Yakobo.



-Je, Mungu alimwambia nini Yakobo alipokuwa bado anaishi Harani?

Tusome Mwanzo 31:13

13- Mimi ni Mungu wa Betheli, huko ulikotia mafuta nguzo, na kuniwekea nadhiri. Sasa ondoka, toka katika nchi hii, urudi mpaka nchi ile uliyozaliwa.

-Je, baada ya Yakobo kuishi Harani miaka mingi, Mungu alimwambia nini Yakobo?

-Mungu alimwambia Yakobo atoke Harani na arejee nchi ya Kanaani.

-Na Yakobo alipokuwa akirejea nchi ya Kanaani, Mungu alimpa jina mpya.

Tusome Mwanzo 32:28

28- Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda.

-Je, jina mpya alilopewa Yakobo ni lipi?
-Israeli.
-Israeli inamaanisha kupambana na Mungu.

-Katika fundisho lifuatalo, tutajifundisha mengi kuhusu Yakobo.